BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 05 Juni, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

118. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Benki nyingi za Biashara zilizopo Tanzania zimejiunga na masoko ya hisa kama vile Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE). Na kwa kuwa ripoti za wataalamu wa fedha zinaainisha faida nyingi za kujiunga na masoko ya hisa. Na kwa kuwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imebaki kando na mwenendo huu na mpaka sasa haijajiunga na masoko haya ya hisa.

(a) Je, ni sababu zipi za kitaalam zinazoifanya PBZ kutojiunga na masoko ya hisa.

(b) Je, ni vipi uamuzi wa PBZ wa kutokujiunga na masoko ya hisa unavyolingana na mikakati ya kifedha na ukuaji wa benki.

(c) Je, PBZ ina mipango au mikakati gani ya baadae kuhusiana

na uwekezaji wa hisa na masoko ya mitaji.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

97. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali kupitia Baraza la Manispaa la Mjini (ZMC) imeamua kubinafsisha maegesho (Parking) yote kwa watoa huduma wa nje ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na kupunguza mianya ya upotevu wa mapato hayo. Hata hivyo, kuna malalamiko mengi kutoka kwa baadhi ya wananchi kuhusiana na utoaji wa huduma katika maegesho mengi yanayomilikiwa na ZMC.

(a) Je, ni kwa kiasi gani ubinafsishaji wa maegesho kwa watoa huduma wa nje umeleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali ukilinganisha na hapo awali.

(b) Je, ni zipi taratibu za kuweza kutenga (Reserve) maegesho kwa matumizi binafsi na ni fedha za kiasi gani Serikali hupata kwa mwaka.

(c) Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuyaboresha maegesho ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wananchi, na ni hatua gani zinachukuliwa kuboresha ufanisi wa utoaji wa huduma hizo.

**Wizara ya Afya:**

163. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Tathmini iko vipi juu ya maradhi ya kisukari kwa Unguja na Pemba.

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi juu ya namna ya kujikinga na maradhi haya.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

42. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kuna taarifa zenye uhakika kwamba wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya Tanzania Bara wakiwemo Wazanzibari wanapofeli hukimbilia Zanzibar katika vyuo hasa vya binafsi (private) vinavyotoa kozi za afya.

(a) Je, ni kwa nini NACTE kwa upande wa Tanzania Bara wawe na mitihani ya pamoja ya vyuo lakini kwa Zanzibar kuwe tofauti kila chuo kijtegemee mitihani yake.

(b) Je, hatuoni kuwa NACTE kwa upande wa Tanzania Bara wanasimamia vyema mtaala na ndio kinachopelekea wanafunzi kufeli na kukimbilia Zanzibar, ambako hakuna usimamizi mzuri wa mtaala.

79. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Sayansi ya Benjamin William Mkapa Tawi la SUZA Pemba inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa Wahadhiri wa kudumu na kulazimika kutumia walimu wa muda wa kufundisha masomo mbali mbali, uvamizi wa maeneo yake na ukosefu wa usafiri wa kudumu kwa walimu na wanafunzi wa skuli hiyo.

(a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inazielewa changamoto hizi.

(b) Je, Wizara yako itachukuwa hatua gani kuziondosha changamoto hizo.

## Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

167. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika hali ambayo miradi mbali mbali mikubwa ya maji inaendelea kusimamiwa na Serikali yetu, kuna vilio vya wananchi wetu vya kukosa maji safi na salama vikiwa vinaendelea. Hivyo, kuna haja kubwa ya kufanya tathmini juu ya ufanisi wa miradi hiyo.

Je, Tathmini ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ya maji iko vipi hadi sasa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

261. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka miundombinu tofauti ili kurahisisha huduma mbali mbali za kijamii. Miongoni mwa miundombinu hiyo ni alama inayoonesha daraja, skuli, 'zebra cross' na nyenginezo. Kwa kuwa alama ya 'zebra cross' inawataka madereva wasimame ili kuwapisha wanaotembea kwa miguu waweze kukata kwa urahisi katika alama hizo, bado madereva wengi hawaziheshimu alama hizi na matokeo yake huwagonga watu kwenye 'zebra cross' na wakati mwengine husababisha vifo.

(a) Je, ni adhabu gani hutolewa kwa dereva anaemgonga mtu kwenye 'zebra cross'.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wa Zanzibar wanaopata majeraha na kupoteza ndugu na jamaa zao kwa tabia za madereva hao.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

207. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni aina gani ya kilimo bora ambacho kinazingatia uhifadhi wa mazingira yetu kwa mustakbali wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

65. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa ya Awamu ya Nane imeanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, ikiwa ni njia moja ya kuukuza Uchumi wa Buluu na Uvuvi hapa nchini. Katika kulifikia lengo hilo, Serikali inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi imefanya maamuzi mazuri ya kuwapatia boti wananchi mbali mbali ili waweze kuzitumia katika kuongeza kasi ya uvuvi nchini.

Ni lini wavuvi hao watapatiwa boti za uvuvi wa kina kirefu cha maji.

III. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Maji, Nishati na Madini:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**05 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**